# Mzizi na Shina: Maswali yasiyo Rahisi[1]

**N.V.Gromova**

**Taasisi ya Taaluma za Kiasia na Kiafrika,**
**Chuo Kikuu cha Taifa cha Moscow Lomonosov**

**Ikisiri**

Makala inachambua na kupendekeza ufumbuzi kuhusiana na vigezo vya kuamua mzizi na shina katika Kiswahili ni nini. Makala inapendekeza kuwa mizizi isiwe -pig-, -som-, jib-, n.k. bali *piga, soma, jibu, nomino, lakini* n.k. na mashina yawe *pishwa, kamilisha, somesha*, n.k. Pendekezo hili ni jipya na linatofautiana na lile lililomo katika SAMAKISA na vitabu vingine vya zamani vya sarufi ya Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Mara nyingi wanafunzi wanatuuliza sisi, walimu wao, maswali yasiyojibika haraka haraka. Maswali huwa yanahusu sarufi maumbo; wanafunzi hutaka kuelewa misingi yake na kanuni zake. Mathalani, wanauliza, kwa sababu gani vitenzi kadhaa vilivyoongezwa viambishi nyambulishi vitendea (kama -*ambia*) vimo katika lugha na vitenzi sahili (-*amba*) vimetoweka ama kutumika kwa nadra tu; kwa nini katika ngeli moja kuna nomino za aina mbalimbali za kisemantiki; mbona vitenzi viwili tu vyenye silabi mbili yaani -*isha* na -*enda* vinatumika na kiambishi awali *ku*-, n.k. Idadi ya maswali kama hayo, yahusuyo sarufi maumbo, haihesabiki; yanadai yafanyiwe uchunguzi wa kina.

Maswali kama hayo yamechochea haja ya kueleza upya misingi ya sarufi ya Kiswahili na tulipotunga kitabu cha Sarufi ya kinadharia ya Kiswahili (kilichotolewa kwa Kirusi) tulijaribu kutoa mitazamo yetu kuhusu mada hizo [Gromova, Okhotina].

---

[1] Makala hii nimeiandika kwa heshima ya marehemu Mwalimu Besha. Mwalimu Besha alikuwa mwalimu mkweli, aliyewapenda wanafunzi wake na kupenda kuwafundisha, tena aliweza kuwaelezea kwa undani na kwa uwazi na wakati huo huo kwa urahisi maswali magumu ya sarufi ya Kiswahili. Nilipata kusikiliza mihadhara yake kwa ajili ya wanafunzi wa mwaka wa tatu mnamo mwezi wa Januari mwaka wa 1990; mada yake ilikuwa ni "Aina za maneno". Nakumbuka alisema kwamba "hakuna njia rahisi za kuainisha maneno katika vikundi". Aliniomba nishiriki katika kutoa mihadhara hiyo na mada yangu ilihusika pia na uainishaji wa maneno. Ingawa misimamo na mikabala yetu ilikuwa tofauti kidogo, lakini tulikubaliana kwa jumla, tukijaribu kuwaelezea wanafunzi wetu vigezo muhimu vya sarufi maumbo.

Katika makala hii ninachofanya ni kujaribu kudokeza jambo moja muhimu ilinalohusu sarufi maumbo ya Kiswahili ambalo linawatatanisha wanafunzi wa lugha hii pamoja na wanaisimu wengine. Nafikiri kwamba ufafanuzi na utatuzi wake utanufaisha ufundishaji wa Kiswahili Sanifu. Swali lenyewe ni: Mzizi unatofautishwa na shina la neno kwa kutegemea vigezo gani? Je, vipashio hivi viwili vina maana gani na uamilifu gani katika neno?

Inaonekana kwamba maswali haya ni mapana, na kama wanavyoandika watungaji wa SAMAKISA "yanahusisha mambo mengi kama vile vigezo vilivyotumika kuamua jambo, mitazamo ya wanasarufi wenyewe au mitazamo ya kinadharia. Matumizi ya vigezo vya aina nyingine huweza kuleta matokeo tofauti kabisa na yale yaliyomo katika kitabu hiki" [SAMAKISA: 3]. Sio nia yangu kupata matokeo tofauti, ninacholenga ni kujaribu kujibu maswali yaliyoulizwa hapo juu ama kujadili kwa jumla uwezekano wa kuyajibu, na kwa hivyo kurahisisha mafundisho ya Kiswahili Sanifu hasa kwa wageni.

Tena, kueleza masuala tata kama hayo kunasaidia kutatua matatizo ya kitaipolojia. Kinadharia taipolojia iitwayo "mbona-taipolojia" [Kibrik] inawezesha kujishughulisha kwa makini na undani zaidi na uchanganuzi na uchambuzi wa maana asilia ya vipashio mbalimbali vya kisarufi.

### 1.1 Viambishi

Kama inavyojulikana, kutokana na nafasi ya viambishi katika neno, lugha ya Kiswahili kina viambishi vya aina tatu yaani viambishi awali, "*viambishi kati*" na viambishi tamati, vyenye umbo la /I / = irabu, au /K/ =konsonanti, ikiwa nazali /m/, /n/, au KI, kwa mfano:

1. kiambishi awali: ***u***-refu (I), ***m***-tu (K), ***tu***-nasoma (KI);
   "*kiambishi kati*": ata-***i***-ona (I), tuli-***m***-penda (K), nime-***ki***-ona kitabu (KI);
   kiambishi tamati: asom-***e*** (I),msoma-**ji** (KI), walikuta-***na*** (KI).

Kusema kweli, "*viambishi kati*" vilivyo halisi havipatikani katika Kiswahili, kwa sababu viambishi kati vilivyo sahihi hujitokeza ama kujiingiza ndani ya mzizi wenyewe wa neno, kama katika lugha ya Yurok, lugha ya wahindi wa Kimarekani wakaao kwenye jimbo la California, neno "shamba" ni *sepolah* na wingi wake ni *se-**ge**-polah* {Robins: 210]. "Katika lugha nyingine za Kibantu viambishi...huweza pia kujitokeza ndani ya mzizi-funge wenyewe" [SAMAKISA: 66]. Lakini wanaisimu wengi wa lugha ya Kiswahili walifuata na mpaka siku hizi wengi wanaendelea kufuata ufafanuzi wa kiambishi kati uliotolewa na C.Doke anayesema kwamba kiambishi kati ni kiambishi

kilichoko kati ya kiambishi awali na mzizi/shina la neno [Aksyonova: 130-131].

Kosa hili ama tuseme dosari hii ya kiistilahi ilikuwa imesahihishwa na watungaji wa SAMAKISA ambao kwa kutegemea nafasi inayochukuliwa na viambishi wanaviita sio viambishi kati bali viambishi awali. Lakini maelezo kama hayo (nafasi za viambishi hivi mwanzoni mwa mzizi: ***tu*** + ***li*** + ***po*** + ***wa*** + ona) [SAMAKISA: 67] hayawezeshi kuelewa ipasavyo tofauti iliyo kati ya vivuli vya maana za kisarufi za mofimu hizi kutokana na mahali pake katika neno. Tulinganishe, kwa mfano, viambishi awali viwili vyenye umbo sawa katika kitenzi ***wa***-li-po-***wa***-ona, ambako kiambishi awali cha kwanza kinaonyesha nafasi ya kiima na kiambishi awali kilichopo karibu kabisa na mzizi kinaonyesha nafasi ya yambwa.

## 1.2 Mzizi wa nomino

Dhana ya "mzizi" ni muhimu sana katika kueleza kila utanzu wa sarufi maumbo ya Kiswahili hasa katika kuelezea njia za uundaji wa maneno, upatanishi, unyambulishaji na uambishaji wake. Kamusi ya isimu na lugha inasema kwamba "Mzizi ni sehemu ya neno ambayo huwa haibadilikibadiliki". Watungaji wa SAMAKISA [63] wanapokea fasili ya David Crystal asemaye kuwa: "Mzizi ni umbo-msingi la neno ambalo haliwezi kuchanganuliwa katika sehemu nyingine ndogo bila kupoteza (uamilifu na) utambulisho wake (wa kisemantiki)". Hivyo inaeleweka kuwa mzizi hauwezi kugawanywa zaidi bila ya kuathiri maana yake.

Kama kawaida wanaisimu wanaposema juu ya mzizi wenyewe wa nomino (ama kivumishi, kielezi, kiwakilishi na aina nyingine za maneno isipokuwa kitenzi) wanakubali kwamba umbo lake ni /KI/ ama /II/ ama /KIKI/ ama /IKI/ ama mpangilio mwingine wa irabu na konsonanti, ikiwemo irabu inayochukua nafasi ya mwisho katika umbo la mzizi. Angalia mifano hii:

2. (KI): m-***tu***, u-***le***,
(II): ma-***ua***, h-***ii***,
(KIKI): wa-***toto***, ma-***zuri***, vi-***tano***,
(IKI): mw-***ezi***, m-***ema***, z-***ake***, n.k.

Hapo linazuka swali juu ya uwezekano wa kuondosha irabu ya mwisho ya mzizi wa nomino (sawa na aina nyingine za maneno), hasa tukizingatia kanuni za uundaji wa vitenzi kutoka katika nomino. Chunguza mifano ifuatayo:

3. *neem**a*** na -***neem**esha*,
*nomin**o*** na -***nomin**isha*,
*sabab**u*** na -***sabab**isha*.

Basi, hizi irabu /a/, /o/, /u/ za mwisho wa mzizi wa nomino zimekwenda wapi? Mbona zimetoweka katika umbo la kitenzi kinachohusika ambacho kilinyambuliwa kutokana na mzizi wa nomino wenye irabu hizo? Hatuwezi kupata majibu katika vitabu vya sarufi vya kimapokeo na hata katika SAMAKISA.

**1.3. Mzizi wa kitenzi.**

Kuhusu nomino zilizonyambuliwa kutokana na vitenzi, wanasarufi wengine wanachanganua mzizi wenye umbo lile lile (yaani KIKI katika mifano ifuatayo): wa-***soma***-ji, u-***pika***-ji, ambako *wa-* na *u-* ni kiambishi awali, *-soma* na -*pika* ni mzizi, na *-ji* ni kiambishi tamati. Lakini wanaposhughulikia mzizi wa kitenzi, wengi wao (karibu wote) wanachanganua mzizi wenye umbo /KIK/ yaani ile irabu ya mwisho /a/ inadondoshwa, kwa mfano: -***lal***-a, ame-***lal***-a, kimem-***lal***-i-a.

Ikiwa kiishilizi /a/ ni kiambishi tamati, basi lazima kiwe na maana maalumu ya kisarufi sawa na viambishi vingine vyote. Lakini tujiulize: maana yake ni nini katika kitenzi chenye asili ya Kibantu? Mara nyingi tunaweza kusoma katika vitabu vya sarufi kuwa hiyo /a/ inaonyesha kategoria ya "infinitive, indicative, imperative"[Meinhof: 96-100] ama "hali ya kuamuru, kauli ya kutenda, kiishilizi cha vitenzi vya asili ya Kibantu" [Kapinga: 145, 152] ama inahusiana na dhamira dhahiri yaani ya kudhihirisha tendo kutendeka [SAMAKISA: 90]. Wanaisimu wengine wanaiainisha irabu hiyo kama "active affirmative suffix" [Wilson: 10], ama "an inflectional suffix" [Welmers: 337]. Hivyo, ikiwa /a/ ni mofimu/kiambishi tamati ambayo ni kijenzi cha hali ya kuamuru, basi ile /a/ ina maana gani katika vitenzi *ni**ki**lala* ama *ni**nge**lala* n.k., vinavyoashiria hali ya masharti? Vile vile /a/ inatumika sio kwa kuonyesha hali ya kutenda tu, bali hali ya kutendwa na ya kutendeka pia. Ile /a/ inajitokeza vilevile ikihusiana na dhamira ya maelezo ya ukanushi, sio dhamira dhahiri tu. Linganisha mifano katika (4) hapa chini:

4. *ilipig**a***, *haikupig**a***
*inapigw**a***, *isingepigw**a***
*imepigik**a***, *itakapopigik**a*** n.k.

Tukitazama mifumo ya mabadiliko ya vitenzi katika Kiswahili tutaona kwamba ile /a/ ya mwisho inapatikana kila mara isipokuwa katika hali

ya kukanusha ya wakati uliopo na katika hali ya kutoa rai au dhamira ya matilaba.

### 1.4. Maana ya /a/ ya mwisho katika kitenzi

Wanaisimu wanaoshikilia kwa dhati wazo la mzizi wa kitenzi kuwa na umbo la KIK wanatoa mifano ya unyambulishaji wa nomino kutoka katika vitenzi kama ifuatayo: u-*som*-***a***-ji, m-*som*-i [SAMAKISA: 96], lakini hawaelezi kwa kuridhisha: mbona katika neno la kwanza ile /a/ imo, na katika neno la pili hudondoshwa? Tena, maana yake ya kisarufi na uamilifu wa irabu hiyo /a/ ni nini katika nomino *usom**a**ji*? Nafikiri kwamba viambishi pekee (u- + -ji, m-+ -i) vinasababisha tofauti za maana ya kisarufi ya maneno hayo mawili, kinyume chake irabu /a/ haileti maana yoyote. Linganisha na mifano mingi mingine ambapo ile /a/ haina uzito wowote katika kunyambulisha nomino kutoka katika vitenzi vyenye viambishi tamati tofauti:

5. *u-ondo**a**-ji* linganisha na *u-ondosh**a**-ji*;
   *m-pend**a** (amani)* linganisha na *m-pendw**a**,* n.k.

Aidha, katika kueleza mnyambuliko wa vitenzi mwandishi wa kitabu kimojawapo cha sarufi, Nkwera anandika hivi: "Kitenzi: *kutafuta*. Shina la asili ni -*tafuta,* na mzizi wake -*tafut*-. Ongeza kiambisho -*na* mwisho wa **mzizi** , utapata -*tafutana*"[Nkwera: 48]). Mwanafunzi yeyote akifuata kanuni iliyoelezwa hapo juu na kukiongeza kiambishi tamati -*na* kwenye mzizi -*tafut*- lazima apate *-*tafutna,* ama sio?

Inapaswa kukumbusha maneno ya Welmers aliyesema juu ya kiambishi tamati /a/ kwamba "no specific meaning can be assigned to /a/" [Welmers: 337].

Tukichagua kigezo cha kimaumbo hiki ama kile kuchanganua mzizi wa neno lazima tuangalie kitumike sawia katika aina zote za maneno bila kujali yakiwa nomino ama vitenzi. Ikiwa wanasarufi hukubaliana kwamba irabu ya mwisho ya nomino isiyonyambuliwa ni kipashio kisichonyimwa cha mzizi wake, mbona wanaiondoa irabu kama hiyo ya mwisho kutoka mzizi wa kitenzi cha asili ya Kibantu?

### 1.5 Kanuni za kupachika viambishi nyambulishi

Utata kama huo usitokee, inafaa kutazama kwa upya umbo la mzizi wa kitenzi katika lugha ya Kiswahili. Kwa maoni yangu, irabu ya mwisho inaingia katika mzizi wa kitenzi na nomino (sawa na aina nyingine za

maneno). Dhana hiyo inathibitishwa na mifano ya mnyambuliko wa nomino kutokana na vitenzi:

6. *-piga > m-piga-ji* (kiambishi awali m- + mzizi wa kitenzi + kiambishi tamati -ji),

   *-lala > -u-lala-ji* (kiambishi awali u- + mzizi wa kitenzi + kiambishi tamati -ji)

Kwa upande wake, unyambulishi wa vitenzi vyenyewe inaonyesha kwa uwazi umbo halisi la mzizi wa kitenzi cho chote chenye asili ya Kibantu:

7. *-pigana < -piga-na* (mzizi + kiambishi nyambulishi kitendanishi), *-fumbata < -fumba-ta* (mzizi + kiambishi nyambulishi kishikanishi),

   *-fungamana < -funga-ma-na* (mzizi + kiambishi nyambulishi kifungamanishi + kiambishi nyambulishi kitendanishi).

Hapo inapaswa kueleza kanuni ya kuongeza viambishi nyambulishi kwenye mzizi wa kitenzi ama wa nomino/kivumishi:

(i) Ikiwa viambishi tamati vinaanzia na konsonanti, mzizi umbo lake haligeuki, na irabu yake ya mwisho inabaki kwenye nafasi yake: (ang. mifano katika (7), *u-singizi + -sha > -singizisha; -refu + -ka > -refuka*;

(ii) Kama viambishi tamati vinaanzia na irabu au viyeyusho /w/ ama /y/, basi irabu ya mwisho ya mzizi hudondoshwa kwa irabu ya kwanza ya kiambishi nyambulishi ambayo huchukua nafasi ya ile irabu ya mwisho ya mzizi, k.m. *-piga + ia > -pig(a)ia > -pigia, -soma + -wa > -som(a)wa > -somwa, -sema + m- + -o > m-sem(a)o > msemo.*

(iii) Kanuni hiyo inahusu pia unyambulishaji wa vitenzi kutoka katika nomino, k.m. *haraka + -isha > -harak(a)isha > -harakisha, nomino + -isha > nomin(o)isha > -nominisha.*

(iv) Tena, kanuni hiyo inatumika katika uundaji wa vitenzi kutoka katika mashina ya kitenzi, yaani kitenzi chenye kiambishi nyambulishi kimoja au zaidi: *-piga + -na* (mzizi + kiambishi nyambulishi kitendanishi) > *-pigana* (shina la kitenzi) + *-isha + -wa* > -pigan(a)ish(a)wa > -piganishwa, *-ona + -eka* (kiambishi nyambulishi kitendeka) > *-on(a)eka > -oneka* (shina) + *-na > -onekana.*

## 1.6 Maumbo ya viambishi nyambulishi

Hivyo, kwa kutegemea uchanganuzi wa mifano iliyotolewa juu inawezekana kuainisha maumbo ya viambishi vya Kiswahili ambayo yanatofautiana mno katika vitabu mbalimbali vya sarufi ya Kiswahili. Unaweza kuona maumbo

ya kiambishi kile kile yakiandikwa kwa namna tofauti tifauti kama hivi: *-an-*, *-ana*, *-na*. Kama ninavyodokeza, viambishi katika lugha ya Kiswahili, hasa viambishi nyambulishi vya vitenzi, vina maumbo yafuatayo:

(a) -na — kitendanishi; kilicho sawa na kiunganishi *na* kinachotumika "kuunganisha vipashio viwili vilivyo na hadhi sawia" [SAMAKISA: 186], k.m.*-piga-na*,

(b) -pa — kianzishi; hakitumiki sana katika Kiswahili cha siku hizi lakini kinapatikana katika msamiati wake, k.m. *-nene-pa*,

(c) -ma — kifungamanishi; hakitumiki katika kuunda vitenzi vipya, lakini kimo katika msamiati, k.m. *-acha-ma*,

(d) -ta — kishikanishi; sawa na viambishi *-pa* na *-ma* hakijitokezi katika vitenzi vingi, lakini bado kimo, k.m. *-fumba-ta*,

(e) -wa — kitendwa; karibu kila kitenzi kinaweza kuongezewa kiambishi hiki, k.m. *-som(a)* + *-wa* > *-somwa*,

(f) -ika/-eka/-ka — kitendeka; alomofu mbili za kwanza zinatumika katika vitenzi ambavyo mzizi wake (ama shina) humalizia na /a/, k.m. *-pit(a)* + *-ika* > *-pitika*, *-som(a)* + *-eka* > *-someka*; alomofu *-ka* inajitokeza katika unyambulishaji wa kitenzi kutoka katika kivumishi kinachomalizia na /i/ au /u/, k.m. *-fupi* + *-ka* > *-fupika*, *-refu* + *-ka* > *-refuka*,

(g) -isha/-esha/-sha -iza/-eza/-za, -ya — kitendeshi; kinatumika sana katika Kiswahili cha kisasa, hasa alomofu tatu za kwanza ambazo hujitokeza katika vitenzi vipya vingi, k.m. *taifa* + *-isha* > *-taif(a)isha* > *-taifisha*, *binafsi* + *-sha* > *-binafsisha* n.k. Alomofu *-ya* hutumika kwa nadra, inawezekana kutaja vitenzi vichache tu vyenye kiambishi kitendeshi hiki, k.m. *-pona* + *-ya* > *-ponya*, lakini inaonekana kwamba -ya ni kiambishi awali, na alomofu nyingine za kiambishi kitendeshi zimejitokeza kama matokeo y mabadiliko ya konsonanti ya mwisho ya mzizi wa kitenzi iliyoathiriwa kwa kiyeyusho /y/,

(h) -ia/-ea — kitendea; kiambishi nyambulishi hiki kina msambao mkubwa katika vitenzi vya Kiswahili,

karibu kila kitenzi kinaweza kuongezewa na kiambishi tamati hicho, k.m. *-pata* + *-ia* > *-pat(a)ia* > *-patia*, *-soma* + *-ea* > *-som(a)ea* > *-somea*,

(i) -ua/-oa kibadilifu; kinaleta maana ya tendo kuwa kinyume, k.m. *-funga* + *-ua* > *-fung(a)ua* > *-fungua*, *-chonga* + *-oa* > *-chong(a)oa* > *-chongoa*.

**1.7 Alomofu za viambishi nyambulishi**

Alomofu za viambishi nyambulishi zenye konsonanti /l/kama zile *-lia/-lea* hujitokeza katika vitenzi ambavyo mizizi yake huishia na irabu mbili, k.m. *-chukua* > *-chukulia*, *-ondoa* > *-ondolea*. Lakini kiotimolojia konsonanti hiyo /l/ ni sehemu ya mzizi wenywe, ambayo katika Kiswahili hudondoka ikichukua nafasi kati ya irabu mbili. Linganisha, kwa mfano, *mkuu* (Kiswahili) na *ikulu* (Kinyamwezi). Hivyo, kitenzi *-chukua* kinatokana na **-chukula*, na kitenzi hiki kinapoambatishwa kwa kiambishi *-ia* eti kinapata 'kukumbuka' asili yake.

Alomofu *-za* inapatikana kama matokeo ya kazi ya kanuni ya kiyeyusho /y/ ya kiambishi kitendeshi *-ya* kuathiri konsonanti tangulizi /l/, k.m.

8. *-kaa/*-kala* + *-ya* > *-kaza*,
*-ingia/*ingila* + *-ya* > *-ingiza*,
*-legea/*legela* + *ya* > *-legeza*,
*-ugua/*-ugula* + *-ya* > *-uguza*.

Vile vile viambishi vyenye irabu mbili kiotimolojia lazima viwe na ile /l/ ndani yao, yaani **-ula/*-ola*, **-ila/*-ela*. Hiyo ndiyo sababu ya kujitokeza alomofu *-iza/-eza* , k.m.

9. -funga + -ua > * *-fungula* + *-ya*> *-funguza*,
*-choma* + *-oa* >**-chomola* + *-y* > *-chomoza*,
*-lipa* + *-ia* > **-lipila* + *-ya* > *-lipiza*,
*-toka* + *-ea* > **-tokela* + *-ya* > *-tokeza*.

Kiyeyusho /y/ inasababisha pia mabadiliko ya konsonanti ya mwisho wa mzizi wa kitenzi kama yale /k/ > /sh/, /t/ > /sh/ ama /p/ > /f/, k.m.

10. *-ruka* + *-ya* > *-rusha*,
-pata + -ya > -pasha,
*-ogopa* + *-ya* > *-ogofya*.

Hivyo, maumbo ya alomofu *-isha/-esha/-sha* yanawezekana kuelezwa pia kuwa ni kazi ya kanuni ya kiyeyusho /y/ kuathiri konsonanti /k/ ya kiambishi kitendeka *-ika/-eka/-ka*. Miundo yake ya kimofimu (ama umbo la ndani) ni hii: awali kitenzi hupata kiambishi kitendeka, halafu huongezewa

kiambishi kitendanishi -*ya*, k.m.

11. *-pita + -ika > -pitika + ya > -pitisha,*
*-soma + -eka > -someka + -ya > -somesha*
*-ondoa + -ka > -ondoka + -ya > -ondosha.*

Sigusii hapo vitenzi vya asili ya Kiarabu ingawa kanuni hizo huwa zinatumika pia katika uwanja huo, na mabadiliko ya konsonanti ya mizizi yake hutokana na mazingira ya kifonetiki sawa na vitenzi vya Kibantu.

### 1.8 Mzizi na shina

Kwa mujibu wa Kamusi ya Isimu na Lugha shina ni "sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi" [KASAILU: 53]. Maelezo pungufu hayo yalikuwa yamesahihishwa na kurekebishwa na watungaji wa SAMAKISA [82-87], lakini hawakuweza kuepukana na matatizo fulani katika fasili yao ya dhana hizo mbili. Mathalani, wanaandika kwamba "shina sahili ni mzizi huru", maana yake dhana ya 'mzizi huru' inahusiana na nomino peke yake, angalia mifano iliyotolewa nao: *jembe, godoro,* n.k. Hivyo, maelezo haya yanashiria kwamba kitenzi hakiwezi kuwa na mzizi huru. Tena, wanaendelea kueleza kwamba "shina changamani ni mzizi na kiambishi". Mifano iliyotolewa inaonyesha shina changamani moja tu yaani '*pig + a*' ndani ya maneno yafuatayo '*pig-i-a, a-li-pig-a, a-ta-pig-i-a*' [SAMAKISA: 86]. Kwa kutegemea fasili kama hiyo haiwezekani kuona tofauti kati ya neno kamili na shina lake. Linganisha shina '*pig-a*' na kitenzi kinachoweza kuwa sio neno kamili tu, bali sentensi nzima '*a-li-pig-i-a.*

Ninavyodhani, shina ni mzizi unaopachikwa kiambishi nyambulishi kimoja au viambishi nyambulishi kadhaa. Kiambishi nyambulishi kinaweza kuchukua nafasi upande wa kushoto ama wa kulia wa mzizi wenyewe, k.m.

12. *ki-ti > ki-ji-ti* (ambapo *-jiti* ni shina),
*-piga > piga-n(a)-ish(a)-wa* (ambapo *-piganishwa* ni shina),
*-vuna >a-na -ji-vun(a)-ia* (ambapo *-jivunia* ni shina).

Viambishi vya aina nyingine ni viambishi vijenzi vya neno ambavyo kazi yao ya kisarufi ni kujenga tungo-neno (ambalo hujidhihirisha katika muktadha wa tungo-kirai, tungo-kishazi na tungo-sentensi) ili kukamilisha maana yake ya kisarufi na ya kileksika, k.m.

13. *-ti > mti, miti, uti, kiti, kitini,*
*-soma > soma!, alisoma, asome, hasomi, aliyetusomea, angesoma,* n.k.,
*-refu > mrefu, kirefu, marefu, virefu,* n.k.

Hivi ni viambishi vya ngeli na idadi, viambishi vya nafsi, vya njeo na hali pamoja na viambishi kanushi. Katika kundi hili linaingia pia kiambishi tamati cha nomino -ni, kwa sababu hakijengi neno jipya, bali kinaonyesha mahali pa nomino hiyo katika mazingira ya kimiundo.

Mzizi unaweza kurudufiwa, k.m. *kumbi-kumbi,* ku-*ruka-ruka,* na shina pia linaweza kurudufiwa, k.m. ali-*pigwa-pigwa.* Lakini swali kuhusu uradidi wa shina la kitenzi lililoambatishwa eti viitwavyo viambishi vya kati, yaani viambishi vinayoonyesha nafsi katika nafasi ya yambwa ama viambishi tamati vya dhamira ya matilaba ama viambishi vikanushi, bado linahitaji lichunguzwe zaidi. Angalia mifano ifuatayo:

14. *usi-**mpige-mpige*** (shina lenye kiambishi cha nafsi na cha dhamira ya matilaba)
    *hawani-ulizi**-ulizi*** (shina lenye kiambishi kanushi).

## 2.0 Hitimisho

Tukitumia vigezo na kanuni za uambatishaji wa viambishi zilizotajwa juu tunaweza kudhihirisha dhana ya 'mzizi' na dhana ya 'shina'. Mzizi ni sehemu ya neno lisilo na viambishi vyo vyote kama ile:

15. *-tu (mtu)* -- nomino,
    *-ema (njema)* -- kivumishi,
    *-soma (alisoma)* -- kitenzi,
    *-angu (langu)* -- kiwakilishi,
    *lakini* --kiunganishi,
    *sana* -- kielezi,
    *labeka* -- kiingizi.

Maneno ya aina za kiunganishi, kielezi na za kiingizi yanaweza kuwa na mzizi-huru. Lakini maneno yote mengine yaani nomino, kivumishi, kiwakilishi na vitenzi yana mzizi-funge, kwa sababu hayawezi kutumika pasi na kuwa na kiambishi awali. Hata ikiwa mofimu = kiambishi awali hakiwakilishwi kimaandishi (pengine kinaitwa kiambishi-fiche au mofimu kapa), maana yake ya kisarufi na uamilifu wake utadhihirishwa katika upatanisho wa kisarufi. Chunguza mifano ifuatayo hapa chini:

16. ***O**-tunda **l**-angu **li**-mo,* ***ma**-tunda **y**-angu **ya**-mo*
    ***O**-balbu **y**-angu **i**-mo,* ***O**-balbu **z**-angu **zi**-mo*

Shina ni mzizi ambao hupachikwa viambishi nyambulishi vile visivyoathiri ama visivyotegemea upatanisho wa kisarufi. Mizizi michache ina silabi moja, wingi wake sawa na mashina na viambishi nyambulishi vina silabi mbili mbili za aina ya KI au II.

Mzizi wa nomino na wa aina nyingine za maneno huwa inaishia na irabu yoyote kati ya irabu tano za Kiswahili, k.m.

17. *maneno, tunda, mbuzi, fungu, debe,*
*nzito, njema, nzuri, ndefu, mweupe,*
*zako, wa, sisi, changu, ule,* n.k.

Mizizi ya nomino inaweza kuishia na kila irabu. Irabu /a/ inapatikana kwa jumla katika asilimia 31 ya nomino zenye asili ya Kibantu. Viambishi nyambulishi vya nomino (-ji, -o, -i, -e, -u/-vu/-fu) humalizia pia kwa kila irabu isipokuwa irabu /a/. Wakati huo huo vitenzi vyote vya Kibantu huishia na irabu /a/ sawa na viambishi nyambulishi vyao vyenye /a/ ya mwisho (taz. katika (1.6.). Na hata vitenzi vya kiarabu vikiambatishwa viambishi nyambulishi vinapata maumbo ya vitenzi halisi vya Kibantu. Hivyo, ile /a/ ya mwisho wa vitenzi inaweza kuhesabika kama alama mahsusi ya kigezo kimojawapo cha aina ya vitenzi [Okhotina, Gromova].

## Marejeo


Aksyonova, I.S., Toporova, I.N. (1990). *Vvedeniye v bantuistiku. Imya. Glagol. (Utangulizi wa Isimu ya Lugha za Kibantu. Nomino. Kitenzi.)* Nauka. Moscow.

Ashton, E.O. (1961) *Swahili Grammar Including Intonation.* Longmans. UK

Gromova, N.V., Okhotina, N.V. (1995) *Teoreticheskaya grammatika yazika suahili (Sarufi ya kinadharia ya lugha ya Kiswahili).* Naslediye. Moscow.

Kapinga, M.C. (1978) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.* TUKI. Dar es Salaam.

KASAILU (1990): *Kamusi ya Isimu na Lugha.* Dar es Salaam.

Kibrik, A.E. (1990) KAK ili POCHEMU? (Ob osnovnom voprose tipologii). [VIPI au MBONA? (Juu ya swali la kimsingi la tipolojia)]. In: Tipologia i grammatika (Tipolojia na sarufi). Nauka. Moscow.

Meinhof, C. (1948) *Grundzuge einer vergleichenden Grammatik der Bantu-sprachen.* Hamburg. Nkwera, F.M.V. (1878) *Sarufi na Fasihi.* Dar es Salaam.

Okhotina, N.V., Gromova, N.V. (1975) *On Formal Features of Category Status of the Root Morphemes in Bantu Languages.* In: Kiswahili, 45/1. Dar es Salaam.

SAMAKISA (2001): Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B, Msanjila, Y.P. *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. Sekondari na Vyuo.* TUKI. Dar es Salaam.

Welmers, W.E. (1973) *African Language Structures.* University of California Press. Los Angeles, London.

Wilson, P.M. (1973) *Simplified Swahili.* East African Literature Bureau. Nairobi, Dar es Salaam, Kampala.